OFISI YA RAIS -TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI CHAMAZI DAY

S.L.P 45565, Temeke - Dar es Salaam

TAREHE……

Simu: 0713-454299

0754-836339

Mzazi wa ……

S. L. P……

……

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHAMAZI DAY WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2021**

A. Ninafurahi kukuarifu kuwa……amechanguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA katika shule hii mwaka 2021, Shule ya Sekondari Chamazi Day ipo umbali wa km13 kusini kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Usafiri wa basi kutoka mjini Mbagala rangitatu unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mbagala rangitatu, nauli ni 400/ kwa mtu mzima, 200 kwa mwanafunzi . Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **04/01/2021** na mwisho wa kulipoti ni tarehe **29/01/2021**.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

SARE ZA SHULE

(a)Sare ya shule hii ni **suruali ya damu ya mzee** kwa wavulana na sketi **blue bahari** kwa wasichana shati ni rangi nyeupe mikono mifupi kwa wote.suruali yenye marinda mawili na sketi yenye marinda ya kawaida.

b)Rangi ya hijab ni rangi nyeupe ,hijab isiyokuwa na urembo.

(c)Mwanafunzi anatakiwa kuwa na madaftari 12 aina ya Counter book.

d) mwanao aje na kamusi ya kiingereza kwa kiingereza

(e)Mwanafunzi awe na Begi la shule

(f) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, soksi nyeupe (wasichana)nyeusi kwa (wavulana)

C. MEDICAL EXAMINATION FORM.(FOMU YA MATIBABU)

Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali . fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti.

D.FOMU YA KUANDIKISHWA

Hii ijazwe kwa umakini na mwanafunzi pamoja na mzazi kama inavyo elekezwa.inahusisha taarifa za mwanafunzi na mzazi/mlezi wake katika maadili

E. FOMU YA AHADI

Fomu hii ni fomu ya ahadi ya uadilifu na utii wa mwanafunzi kwa muda wote atakapo kuwepo hapa shuleni. Pia fomu hiyo itahusu ahadi ya mzazi kutoa ushirikiano kwa uongozi wa shule na kumlea mwanafunzi katika maadili yanayofaa.

F.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 mwaka 1978 na kama ilivyorebishwa sheria namba. 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na,teknologia na mafunzo ya ufundi,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RaisTamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Aidha mwanafunzi atakabidhiwa sheria, kanuni na taratibu za shule hii azisome kwa makini.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule ni eneo linalotoa mazingira mazuri ya kumwezesha mwanafunzi kusoma na kupata Elimu. Ili malengo yaliyowekwa yaweze kutimizwa hakuna budi ziwepo sheria na taratibu zitakazolenga wahusika. Ni lazima wahusika wazielewe na kutii kwa kadiri inavyoelezwa.

1.MIPAKA YA SHULE

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujua eneo lote la shule na mipaka yake. Maeneo yafuatayo yanahesabika pia kuwa ni nje ya mipaka ya shule.

(a) Chumba cha Walimu (staff room) na vyumba vya idara mbalimbali
(b) Maabara ya sanyansi
(c) Ofisi za utawala na ghala zote
d)Jikoni
e)Maeneo ya miradi
f) Nyumba za walimu
g) Nje ya Dar es salaam.

2.RUHUSA YA KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE AU NJE YA DAR ES SALAAM

a)Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda furani tu wa siku inatolewa na mwalimu wa zamu kwa kibali maalum.
b)Ruhusa ya kutoka nje ya dares salaam itatolewa a mkuu wa shule au makamu mkuu wa shule kwa kibali maalum
c) Ruhusa ya nje ya shule mwanafunzi anapaswa kuwahi kurudi
d)Ruhusa ya kwenda hospitali anaanzia kupewa cheti kutoka kwa patron/ matron wa shule au mwalimu wa malezi au wa zamu

3.NGUO RASMI ZA SHULE

i.SARE YA SHULE

(a)Suruali kwa (wavulana) na iwe imeshonwa kwa kuzingatia maagizo ya kujiunga na shule. Suruali za kubana "modo" haziruhusiw,.suruali ivaliwe na mkanda mweusi wa ngozi. Sketi kwa wasichana yenye mshono kulingana na maagizo ya shule.
b)Shati jeupe lenye mikono mifupi. Lisilo bana.
c)Viatu vya ngozi **vyeusi** kwa wavulana na **vyeusi** kwa wasichana na visivyo na visingino virefu na vivaliwe na soksi.
d)**Soksi** ndefu **nyeupe** kwa (wasichana) na **nyeusi** (wavulana)

e)Hijabu kwa wanafunzi waislamu, wanaopenda. Hijabu (Punjab dress) iwe pana,ndefu inayofika magotini, ivaliwe na sketi ndefu (siyo suruali) inayofika kwenye viwiko vya miguu.

ii. UVAAJI WA SARE

Sare ya shule ivaliwe katika mazingira yafuatayo:
a) Wakati wa masomo
b)Mwanafunzi atokapo nje ya shule
c)katika mikutano yote ya shule na mikutano ya hadhara

e)ziara ya masomo.

iii.UNADHIFU

a)muda wote sare iwe safi na iliyonyooshwa

b)Wavulana wote wakate nywele ziwe fupi. Hairuhusiwi kusuka zaidi ya mistali saba na siyo chini ya mistari mitano kwa wasichana

iv. MAHUDHURIO

a) Kila mwanafunzi yampasa kuhudhulia vipindi vyote vya masomo vya ndani na nje ya darasa kama ilivyoonyesha kwenye ratiba na kufanya kazi za darasani..

b) Ni lazima kutii kengele au wito wa shughuli yoyote ya shule kwa haraka bila kuchelewa.

c)Kuhudhuria zamu za kuja shuleni wakati wa likizo au jumamosi kama itaamuliwa iwe hivyo

d)wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria na kushiriki katika shughuli zote za shule kama vile baraza la shule,ukaguzi wa usafi,kupandisha bendera ya Taifa,na kazi za mikono na zile atazopangiwa na mwalimu.

4.MALI NA VIFAA VYA SHULE.

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza kwa uwezo wao wote mali na vyombo vya shule vilivyo chini ya uangalizi wao.

a)Hakuna chombo au kifaa cha aina yoyote kinachoruhusiwa kutoka mahali pake kwa matumizi au shughuli zisizo idhinishwa.

b)Iwapo chombo kimehamishwa kwa shughuli maalumu nilazima kirudishwe mahali pake mara tu baada ya matumizi husika.

c) Uharibifu au upotevu wa kifaa chochote cha shule kwa makusudi ama uzembe lazima ufidiwe na muhusika.

5.MATIBABU.

a)Huduma ya kwanza itatolewa shuleni.

b)Inapobidi kwenda nje ya shule kwa ajili ya matibabu ni lazima kuwe na ruhusa kutoka kwa mwalimu wa zamu.

c)Shule haitawajibika na gharama zilizotumika/ zitakazo tumika kumtibu mwanafunzi katika zahanati/ hospitali ya binafsi/ serikali nje ya shule.

6.LUGHA YA MAWASILIANO.

Lugha rasmi kwa maandishi au kwa kuzungumza shuleni ni kiingereza. Hivyo tumia kingereza wakati wote.

7.VITU VISIVYORUHUSIWA.

1.Pete
2.Kunyoa nyusi
3. Herein
4.Kupaka hina
5.Rangi za kucha
6. Kucha ndefu
7. kupaka piko(rangi nyeusi) kwenye nywele/ upara
8. Hairuhusiwi kunyoa kipara
10. Hairusiwi kunyoa mitindo
11. Hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vianavyofanana na jeshi.
12. Hairuhusiwi kuvaa sandozi,viatu vya mikanda isiyoendana na vazi la shule.
13. Mashati makubwa sana na slim fiti hayaruhusiwi.
14. Simu ya mkononi hairuhusiwi.

15.Hairuhusiwi huja na redio shuleni.
16. Huruhusiwi kuja na “game” shuleni.
17.Hurusiwi kuja na cd wala flash shuleni.

8.MWENENDO MWEMA NA NIDHAMU:

i) Msalimu mwalimu kwa heshima wakati wowwote unapoonana naye hasa kwa mara ya kwanza kwa siku hiyo na mpokee chochote alichobeba.
ii)Usizungumze na mwalimu ama mtu anayekuzidi umri wakati mikono iko mfukoni, kiunoni,ama kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani ya jua au kutafuna kitu mdomoni .huo ni ukosefu wa adabu.
iii)Usibishane na mwalimu au kiongozi yoyote bila sababu maalum.Uwamuzi wa mwalimu ni wamwisho pamoja na hayo mwnafunzi anayo nafasi ya kujitetea.
iv)Usifanye kelele za fujo au ghasia katika sehemu zinazohitajika ukimya kama vile ofisini, darasani, maabara, maktaba na kwenye gwaride.
v)Usiwe mchafu kimwili au kimavazi uwe na nywele fupi bila kunyoa kipara,ndevu,masharubu zinyolewe kwa wembe. Uwe nadhifu muda wote.
vi)Usivute sigara, bangi, wala usitumie madawa ya kulevya na usinywe pombe au aina yoyote ya kilevi.
vii)Usicheze kamari, karata wala draft au michezo mingine isiyoruhusiwa shuleni.
viii)Timiza wajibu au kazi uliyopangiwa, na fanya majaribio na mazoezi yanayotolewa darasani.
ix)Usitumie lugha ya matusi, uhuni na mitindo isiyokubalika.
x)Onyesha heshima kwa walimu na raia wengine wote
xi)Usikae ndani au karibu ya vilabu ,baa ya pombe hata kama hunywi pombe.
xii)Usiandike mahali pasipohusika kama vile ukutani,vitabuni, chooni, darasani au kwenye samani, majina yasiokubalika hayaruhusiwi.
Xiii)Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako ama hata mtu mwingine yeyote.
xiv)Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo,uongozi, maandamano,uwakilishi n. k.
xv)Usifanye biashara yoyote shuleni.
xvi)Usichelewe shule kutoka likizo na usipitishe siku za ruhusa ya kuwa nje ya shule.
xvii)Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.
xviii) Hotuba zote lazima zionwe na mkuu wa shule kabla ya kutolewa katika hadhara yoyote shuleni.
xix)Usifanye mkutano bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na kukilea kikundi husika.
xx) Usihubiri dini au siasa au jambo lolote ,sala zote zifanyike mahali panapo husika au palipohusika na utawala kisheria.

9. ADHABU

i)Adhabu zinawezwa kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anayeonyesha utovu wa nidhamu.
ii)Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mwanafunzi ili mradi asipige kiboko au kuzuia kuingai darasani wakati wa masomo.
Iii)Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jadala la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za adhabu . hata hivyo mkuu wa shule ataidhinisha adhabu zinazotolewa kwa mwanafunzi

10.MAKOSA HAYA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHWA KUFUKUZWA SHULENI BILA ONYO AU BILA KUJALI TABIA YAKO YA NYUMA:

1. Kuiba
2. Kufanya mapenzi
3. Ulevi wa aina yoyote
4.Uuzaji bangi au sigara,kucheza kamari.
5. Kumpiga mwanafunzi,mfanyakazi au mtu wa familia wa mwalimu au mfanyakazi
6. Kudharau bendera ya taifa au wimbo wa taifa au wimbo wa shule au alama nyingine yeyote ya taifa
7. Kuchochea mgomo wa aina yeyote au kufanya fujo ya kuhatarisha amani na usalama penye kundi la watu.
8. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu yeyote.
9. Kutofanya mitihani ya shule au ya Taifa.
10. Kumnyanyasa mwanafunzi mwenzio kwa sababu ya ugeni wake au jinsia yake au umbile lake au dini yake au hali yake nyingine yoyote
11.Kukataa kutii amri ya mwalimu au mkuu wa shule.
12.Utoro kutohudhuria vipindi darasani au kukaa vichakani "chimbo"
13. Kukutwa na vitu vyenye ncha kali kama vile:kisu,bisibisi,nk katika mazingira ya shule.

……

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI CHAMAZI

S.L.P 45565, Temeke - Dar es Salaam

Picha ya mwanafunzi

D.FOMU YA KUWANDIKISHWA

(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi)

1.Jina la mwanafunzi……

2.Uraia……

3.Dini……

4.Tarehe ya kuzaliwa……

5.Mahali ulipozaliwa……

6 Yatima/sio yatima/mzazi mmoja kata isiyohusika……

7.Shule uliyosoma kabla ya kuja Secondary ya Chamazi (Jaza jedwali)

JINA LILIOANDIKISHWA	**SHULE YA MSINGI ULIKOSOMA**	**MWAKA ULIOANZA**	**MWAKA ULIOMALIZA**

Picha ya Mzazi /Mlezi

SEHEMU HII IJANZWE NA MZAZI/ MLEZI

1.Jina la Mzazi……
2. Urai……
3.Anuali kamili Mjini DSM……
4 Sehemu unayoishi Wilaya……
5. Mtaa……
6 Kata……
7 Namba ya simu……..
Je mtoto anamatatizo ya
kiafya……

9.Je anatakiwa uangalizi wa ziada ndiyo ☐ Hapana ☐ -tick lililo sahihi

Kama jibu ni ndiyo toa maelezo mafupi.
……
MAELEZO MENGINE

1.Ni wangapi kuzaliwa……

2.Idadi ya kaka…….

3.Iidadi ya dada……

4.Baba yu hai- ndiyo/Hapana

Mama yu hai- ndio/ Hapana
5. Mtoto analelewa na …….. na……
6. Kazi ya baba……..... simu na……..
7. Kazi ya mama……..simu na…….
8.Kazi ya mlezi……..……. simu na…….

NB: Shauri lolote la Mwanafunzi litatarajiwa kufuatiliwa na Mzazi au Mlezi wake anayetambulika na Shule na siyo mtu yeyote yule kama inavyooneshwa katika jedwali hili.

NO	JINA LA MZAZI/MLEZI	MAHALI ANAPOISHI	NAMBA YA SIMU	NAMBA YA SIMU	UHUSIANO
1					
2					
3					

E.FOMU YA AHADI

AHADI YA MWANAFUNZI

MIMI (JINA KAMILl)……

1.Nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote na nimekubali kujiunga na Shule hii ya Sekondari ya Chamazi tarehe……..

2. Naahidi kwamba:

(a) Nitazingatia sheria zote za Shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa

(b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Serikali ya Jamhuli ya Muungano ya Tanzania

(c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu na vifaa vya maabara na alam za Taifa

…… ……..

Saini ya mwanafunzi Tarehe

AHADI YA MZAZI /MLEZI

Mimi……Mzazi /Mlezi wa …….kidato cha…….....nahidi kwamba:

(a) Nitashirikiana na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa atazitii sheria zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa na mwanangu ataingia kusoma vipindi vya dini ya …….dhehebu la……

(b)Nitafanya kila niwezavyo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku kabla y saa 1.00 asubuhi.

Nitafuatilia maendeleo yake Shuleni aidha nitaitika wito wowote toka shule. Na kwamba mwanafunzi atahudhuria Shule kuanzia kidato cha Kwanza hadi cha Nne kwa juhudi zangu binafsi, Mwanafunzi na Walimu wake.

Saini ya Mzazi/Mlezi……Tarehe……./…20……..

TEMEKE MUNICIPAL
CHAMAZI DAY SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 45565, TEMEKE DAR ES SALAAM

FORM FOR STUDENTS MEDICAL EXAMINATION

Please examine
Name in Full…….
To his/her physical and mental fitness, for a full time student at CHAMAZI sec school. The examination should include the following categories:
EYE SIGHT HERING LIMBUS DISEASES
LEPROSY PREGNANCY
……..
HEADMISTRESS
MEDICAL CERTIFICAL

(To be completed by a government medical officer)
I have examined the above and consider. Physical* fit/unfit and mentally

Fit/ unfit for full time Academic training course.
1.. Eyesight…….
2. Hearing…….
3.Limbs……..
4.Leprosy……
5. Epilepsy…….
6. Neurosis……
7. Pregnancy……
8. Other series disease……
9. Medical officer comment……..

Date……/……../……

Station……

Designation……